



Tovuti: www.nsimbodc.go.tz

Nsimbo Wiki hii

Tunatekeleza

NSIMBO
DISTRICT
COUNCIL

TOLEO NA.06

MACHI 8 , 2019

RC Makala asisitiza Ushirikiano Wananchi, Viongozi Nsimbo,

- ◆ Awataka Wananchi Kanoge kuacha Woga,kuwa wawazi,
- ◆ Amwagiza DC kuchukua hatua kali dhidi ya Mvamizi wa Ardhi "Masanja",
- ◆ Awakumbusha kuzingatia Sheria Makabidhiano,Mauziano ya Ardhi,

SomaUk.2



Pichani : Mkuu wa Mkoa wa Katavi Mh.Amos Makala (Wa kwanza kushoto) akisikiliza Maelezo kuhusu eneo la Mgogoro kutoka kwa Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo Bw.Betvely Ruhega (Wa kwanza upande wa kulia) wakati wa Ziara ya Mkuu huyo wa Mkoa Machi 4,2019 kutembelea eneo hilo la Mgogoro wa Ardhi kati ya Wananchi wa Kijiji cha Tumaini Katika Kata ya Itenka na Mtu almaarufu "Masanja"anayedaiwa kuvamia Ardhi Kijijini hapo .(Picha na:John Mganga)

RC Makala asisitiza Wananchi Ushirikiano kwa Viongozi..

Na:John Mganga

Nsimbo-Itenka,

Mkuu wa Mkoa wa Katavi **Mh.Amos Makala** ametoa wito kwa Wananchi Nsimbo kuwa wakweli na wawazi na kutoa ushirikiano kikamilifu kwa Viongozi ili kurahisisha utoaji maamuzi kwa haki na kwa wakati katika masuala mbalimbali likiwemo suala la utatuzi wa Migogoro ya Ardhi.

Mkuu wa Mkoa Ameyasema hayo Machi 4, 2019 katika Kata ya Itenka Kijiji cha Jilabela alipofanya ziara ya kikazi akiambatana na Kamati yake ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa na Kamati ya ulinzi na usalama ya Wilaya kutembelea Maeneo hayo kwa lengo la kusikiliza na kutatua kero za Wananchi.

Awali kabla ya kuanza kuzungumza na kusikiliza kero za Wananchi Mh.Makala ali-

tembelea eneo lenye Mgogoro wa Ardhi katika Kijiji cha Tumaini, Mgogoro unaohusu Wananchi dhidi ya Mtu anayedaiwa kuvamia Mashamba ya Wakulima, kwa lengo la kujionea na kujiridhisha na hatua ambazo zimekwisha chukuliwa.

Akizungumza na Wananchi hao wa Kata ya Itenka Mh.Makala amesema kiten-do cha Wananchi kutokuwa wakweli na wawazi kwa Viongozi wa ngazi za Vijiji, Kata, Wilaya na hata Mkoa wakati wa utoaji maelezo ndiko kumekuwa sababu kubwa ya kucheleweshwa utoaji maamuzi katika mashauri mbalimbali yakiwemo Mashauri yahasuyo Migogoro ya Ardhi.

Mh.Makala aliyasema hayo kufuatia kuwepo kwa Malalamiko yaliyotolewa na Wananchi katika Mkutano huo dhidi ya mtu anayedaiwa kuwa Mvamizi wa Maeneo ya Kilimo ya baadhi Wananchi Kijijini hapo anayetambulika kwa Jina la "Masanja" kuendelea kushikilia mashamba ya Wakulima hao na kuyatumia kwa shughuli za Kilimo licha ya shauri

hilo kutolewa uamuzi katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mpanda.

Kufuatia malalamiko hayo Mkuu wa Mkoa wa Katavi akatoa wito kwa Wananchi Kijijini hapo kuwa wawazi na kutoogopa kueleza ukweli kwa kuwa katika Nchi ya Tanzania haku-na mtu aliye juu ya Sheria na kwamba endapo suala hilo lingekuwa limetolewa maelezo ya kujitosheleza hatua madhubuti zingekuwa zimekwisha chukuliwa.

Aidha Mh.Mkuu wa Mkoa amemuagiza Mkuu wa Wilaya ya Mpanda Bi.Lilian Charles Matinga kuhakikisha kuwa anamchukulia hatua za Kisheria mtu huyo anayedaiwa kuendelea kushikilia Mashamba ya Wananchi Kijijini hapo na kuyatumia kwa shughuli zake za kilimo licha ya shauri hilo kutolewa Maamuzi katika ofisi Mkuu wa Wilaya.

Amesema kitendo kinachofanywa na Mvamizi Masanja ni cha kudharau Mamlaka za Serikali na kwamba kitendo hicho kamwe hakitavumilika.

Katika hatua nyingine Mh.Makala ametoa wito kwa Wananchi kutotafsiri Agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh.Dr.John Magufuli la kuendelea na shughuli za Kijamii katika maeneo ya hifadhi yaliyopigwa marufuku kwa kuvamia maeneo hayo na badala yake kusubiria utaratibu utakaotolewa na Halmashauri kupitia Idara ya ardhi ili kuwawezesha kurejea katika maeneo hayo na kuendelea na shughuli zao za Kiuchumi kwa utaratibu mzuri utakaotolewa. *Inaendelea uk 3.*



Pichani:Mkuu wa Mkoa wa Katavi Mh.Amos Makala akizunguma na Wananchi wa Kata ya Kanoge Machi4,2019 katika ziara yake Katani hapo kwa lengo la kusikiliza na kutatua Kero za Wananchi.(Picha na Jonh Mganga)

RC MakalaInatoka uk.2

Tahadhari hiyo inatolewa na Mkuu wa Mkoa kufuatia baadhi ya Wananchi kutafsiri tamkoa la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Vibaya na kuvamia maeneo yaliyopigwa marufuku na kuendelea na shughuli zao ambapo baadhi yao wamekuwa wakiendelea kufanya uvamizi zaidi katika maeneo mengine zaidi.

Mbali na hilo, Makala amewataka wananchi wa Kata ya Itena kutumia vema fursa ya kilimo cha Mpunga kujitelea maendeleo ikiwemo Ujenzi na uimarishaji wa Miundombinu ya Afya kama vile Zahanati pamoja na Upanuzi wa Miundombinu ya Madarasa kwa ajili ya shule

ili kuinua kiwango cha elimu katika Kata hiyo.

Mh.Makala ameyasema hayo kufuatia kutembelea eneo hilo la Itenka na kujionea bonde kubwa la Mpunga ambalo ndio linalotegemewakwa sehemu kubwa na wakazi wa Itenka katika kilimo cha Mpunga

Pamoja na mambo mengine Mkuu wa Mkoa Mh.Makala amewatoa ho-fu Wananchi juu ya changamoto ya ubovu wa Barabara ya Mpanda Itenka ambayo katika baadhi ya maeneo imekuwa na ubovu ambapo amesisitiza kuwa changamoto hiyo itapatiwa ufumbuzi muda mfupi ujao kwa kuwa amekuwa akifanya na anaendelea kufanya mawasiliano

ya karibu na Meneja wa TARURA Mkoa ili kumaliza tatizo hilo.

Aidha Mh.Makala pia amewahakikishia Wananchi wa Itenka kuwa Umeme katika eneo hilo utafika kwa kuwa amekuwa akifanya mawasiliano kwa karibu na Meneja wa Shirika la Umeme TANESCO Mkoa wa Katavi ili kuharakisha upatikanaji wa umeme katika eneo hilo ambapo tayari baadhi ya nguzo zimekwisha simikwa kwa ajili ya kufikisha umeme katika Kata hiyo.

Mkuu wa Mkoa wa Katavi Amos Makala anafanya ziara yake Itenka ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Ratiba yake ya Mwezi aliyojiwekea kutembelea na kusikiliza na kutatua kero za Wananchi,

Wananchi Kanoge wapongeza Elimu Mabaraza ya Kata

Wananchi wa Kata ya Kanoge Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo wameipongeza Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo na Kitengo cha Sheria kwa kuratibu na kutekeleza Mpango kazi wa utoaji wa Elimu kwa mabaraza ya usuluhishi ya Kata za Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo.

Akizungumza kwa niaba ya Wananchi katika uzinduzi wa shughuli ya utoaji wa Elimu kwa mabaraza ya usuluhishi ya Kata yaliyotolewa Machi 1,2019 Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo na Diwani wa Kata ya Kanoge Mh.Salehe Msompola amesema ni jambo la kufurahisha kwa Halmashauri kuandaa na kutekeleza Mpango kazi wa utoaji wa Elimu kwa mabaraza hayo ya Kata

Amesema Elimu hiyo kwa Kata ya Kanoge inatolewa kwa muda muafaka kutokana na ukweli kwamba kwa muda mrefu Elimu hiyo haijatolewa kwa Mabaraza ya Kata jambo ambalo limekuwa likiathiri kwa kiasi kikubwa Usikilizaji, usuluhishi na utoaji wa haki katika Kata hiyo.

Ameongeza kuwa kutokana na Elimu hiyo kutotolewa kwa wakati Wajumbe wa Mabaraza ya Kata hususani wa Kata yake wamekuwa wakifanya Maamuzi na kusuluhisha Migogoro mbalimbali katika Jamii pasipo kujua mabadiliko ya sheria mbalimbali zinazopaswa kuzingatwa na kusimamiwa katika utoaji wa Maamuzi jambo ambalo wakati mwingine limekuwa likiathiri kwa sehemu kubwa utoaji wa haki.

Makamu Mwenyekiti Msompola amesema ikiwa Elimu hiyo itatolewa mara kwa mara katika Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo itasaidia kwa kiasi kikubwa mabaraza hayo ya usuluhishikuwa na uelewa wa Mabadiliko ya Sheria mbalimbali zikiwemo sheria za Ardhi.

Kutokana na Fursa ya Elimu ya Sheria kwa baraza la usuluhishi la Kata Kanoge, Makamu Mwenyekiti Msompola ametoa wito kwa Wajumbe wa Baraza hilo kuzingatia Sheria Kanuni na Taratibu za Nchi wakati wa utoaji maamuzi katika mashauri mbalimbali wanayofanyia usuluhishi ili kuhakikisha kuwa haki inatendeka

InaendeleaUk.4.

Inatoka Uk..3

Elimu ya Sheria kwa mabaraza ya Kata Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo inatolewa ikiwa ni utekelezaji wa Mpango kazi wa Kitengo cha Sheria chini ya Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo wa kuyajengea uwezo juu ya uelewa wa Sheria Mabaraza ya Kata zote 12 za Halmashauri.

Tayari Elimu hiyo imekwisha tolewa kwa Wajumbe wa Mabaraza ya Usuluhishi ya Kata za Nsimbo, Kapalala, Mtapenda na Kanoge ambapo mabaraza ya Kata zingine yataendelea kujengewa uwezo kwa mujibu wa ratiba iliyoopo.



Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo na Diwani wa Kata ya Kanoge Ndg. Salehe Msompola akizungumza wakati wa ufunguzi wa Mafunzo ya kuyajengea uwezo mabaraza ya Kata yaliyotolewa Machi 1, 2019 katika Ofisi ya Mtendaji Kata ya Kanoge.

Wananchi Nsimbo watakiwa kuchukua tahadhari Mapema dhidi ya Majanga

Na: John Mganga, Nsimbo HQ

Wananchi Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo wametsakiwa kuchukua tahadhari mapema dhidi ya majanga mbalimbali yanayotokea katika taasisi binafsi, makampuni, taasisi za kiserikali, Taasisi za Dini pamoja na nyumba Binafsi ili kuepusha athari zinazoweza kusababishwa na majanga hayo.

Rai hiyo imetolewa na Mratibu wa Maafa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo Bw. Saimon Kajange Machi 8, ofisini kwake kufuatia Maafa yaliyotokea katika chuo cha Maendeleo ya Wananchi Msaginya kufuatia Moto uliotekeza Bweni la Wavulana na kusababisha Hasara ya Jengo na Mali za Wanachuo kuteketea kwa moto.

Bw. Kajange ameeleza kuwa Majanga mengi ya Moto katika Maeneo mbalimbali Nchini yamekuwa yakileta athari kutokana na taasisi mbalimbali, ama nyumba za kuishi kutokua na Vifaa vya tahadhari dhidi ya Janga la moto hali inayopelekea pindi moto unapozuka wahusika kushindwa kuudhibiti na hivyo kusababisha madhara mbalimbali ikiwemo kuteketea kwa Mali, na wakati mwingine kusababisha vifo.

Kajange ameongeza kuwa kutotoa taarifa kwa wakati pindi Majanga mbalimbali yanapotokea hususani Janga la moto imekua sababu kubwa inayosababisha kuleta athari zitokanazo na Majanga ya Moto.

Amesisitiza kuwa ni muhimu taasisi mbalimbali binafsi na za serikali pamoja na mashirika na

nyumba za watu zikawa na utaratibu wa kuweka vifaa mbalimbali vya tahadhari ili kukabiliana na Majanga pindi yanapotokea.

Akizungumzia kuhusu tukio la Moto uliotokea katika chuo cha maendeleo ya Wananchi Msaginya Kajange emeeleza kuwa ni muhimu kwa uongozi wa Chuo kuhakikisha kuwa majengo yote ya chuo ikiwemo mabweni yanakua na vifaa vya kukabiliana na moto pamoja na kuhakikisha kuwa elimu juu ya matumizi ya vifaa hivyo vya kuzimia moto yaani fire Extinguisher inatolewa kwa wanafunzi ili kukabiliana na Majanga ya moto.

MATUKIO KATIKA PICHA



Picha Na.1.Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Katavi akizungumza na Wananchi wa Kata ya Kanoge katika Ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Katavi Mh.Amos Makala Mchi 4,2019, iliyofanyika kwa lengo la kusikiliza kero za Wananchi



Picha Na.2.Wananchi wa Kata ya Itenka wakimsikiliza Mkuu wa Mkoa wa Katavi Amos Makala wakati wa Mkutano na Wananchi hao Machi 4,2019 katika ziara yake yenye lengo la kusikiliza na kutatua kero za Wananchi



Picha No 3.Mama Mwenye ulemavu wa Miguu akiwasilisha kero yake Mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Katavi Mh.Amos Makala katika Ziara yake aliyofanya Machi 4,2019 katika Kata ya Itenka kusikiliza kero za Wananchi



Picha No 4.Mkuu wa Wilaya ya Mpanda Bi Lilian Charles Matinga akisalimiza wananchi wakati wa Ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Katavi katika Kiata ya Itenka Machi 4,2019



Picha No 6. Mkuu wa Mkoa wa Katavi Mh.Amos Makala akisalimiana na baadhi ya Wananchi mara baada ya mkutano wake katika Kata ya Itenka kuzungumza na Wananchi.



Picha No 5.Injinia wa Ujenzi Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo Bw.Golden Katoto (Mwenye shati jekundu)akifafanua jambo mbele ya Diwani wa Kata ya Katumba Seneta Baraka(Mwenye T.Shirt nyeusi) wakiwa Site ya Ujenzi



Picha No 7. Akiwakilisha Watumishi Wanawake Nsimbo Bi Florentina Ilumba akikabidhi Msaada wa Chakula kwa Watoto Yaimea wa Kituo ca Getsemane kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo Mchi 8,2019.Watumishi wanawake Nsimbo wameadhimisha siku yao kwa kutembelea Kituo hicho.



Jarida hili la Wiki Nsimbo huandaliwa na kutolewa na
Kitengo cha Teknolojia ya Habari Mawasiliano na
Uhusiano Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji ,Halmashauri
ya Wilaya ya Nsimbo,Ofisi Na.2

Mawasiliano:

Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo

SLP 688,Mpanda Katavi

Barua pepe:info@nsimbodc.go.tz

Tovuti:www.nsimbodc.go.tz

Tel +25546310716